**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

Mtaa wa Maweni /Mjimwema
Barabara ya Soko Maziwa/Tungi
Simu namba:
**Barua pepe:** aboudajss@gmail.com

Shule ya Sekondari Aboud Jumbe
S. L. P 10956
**Dar Es Salaam**
**Tarehe: ………………………**

Kumb. Na. AJSS/JI/ F.5/ 2022/2023
JINA LA MWANAFUNZI ……………………….............
**S.L.P**
……………
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ABOUD JUMBE WILAYA YA KIGAMBONI MWAKA 2022/2023</u>**

**1.0.** Nina furahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na **KIDATO CHA TANO katika Shule ya Sekondari Aboud Jumbe. Shule ipo umbali wa km 6 kutoka Ferry. Eneo la Kisota Mjimwema - Kigamboni. Usafiri wa basi kutoka Ferry unapatikana kituo cha mabasi Ferry unashuka MAWENI au basi za TUNGI unashuka Mnadani.** Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe ……………….. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………….. kwa ajili ya usajili akiwa na vifaa vyote**. [Siku ya kufungua Shule usajili hautafanyika].**

**NB:KIKAO CHA WAZAZI KITAFANYIKA TAREHE …………………….. SAA 03:00 Asubuhi – FIKA NA MWANAFUNZI.`**

**2.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule ya Sekondari Aboud Jumbe yenye namba ya usajili namba 1674 inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini,unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa siku ya kuripoti Shuleni.

i. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio ni lazima katika kila shughuli za ndani na nje ya shule
iii. Kutimiza kwa makini maandalizi yake ya kila siku.
iv. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine zote utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare za shule wakati wote unapokuwa kwenye mazingira ya shule.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

ix. Kuwahi shuleni ambapo mwanafunzi anatakiwa kufika saa 12:30 asubuhi.

**3.0. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Uasherati, Ubakaji na Ushoga.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
5. Uvutaji bangi
6. Makosa ya jinai
7. Kupigana au kupiga
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
9. Kudharau bendera ya Taifa.
10. Kuoa au kuolewa
11. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
12. Kutoa mimba.
13. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
14. Kukataa adhabu kwa makusudi
15. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu awapo shuleni, ikikamatwa **HATARUDISHIWA.**
16. Kutokufanya mitihani bila sababu yoyote ya msingi.
17. Kuwa nje ya eneo la shule wakati wa masomo.

**3.1. ADA NA MICHANGO KWA WANAFUNZI WA KUTWA MCHEPUO WA HGL, HGK MCHANGANUO UFUATAO UNAONYESHA**

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Ada | - 20,000/= |
| (ii) | Taaluma | - 20,000/= |
| (iii) | Kitambulisho na picha | - 5,000/= |
| (iv) | Tahadhari(Haitarudishwa) | - 5,000/= |
| (v) | Ukarabati wa samani | - 15,000/= |
| (vi) | Huduma ya kwanza | - 5,000/= |
| (vii) | Mtihani wa Mock | - 20,000/= |
| (viii) | Nembo | - 4,000/= |
| (ix) | Vibarua | - 4,000/= |
| | **JUMLA** | **98,000/=** |

Ada na michango yote ipelekwe Benki kwenye Akaunti ya shule. Jina la Akaunti ni **ABOUD JUMBE SECONDARY SCHOOL, Namba ya Akaunti 20703500462 NMB – TEMEKE BRANCH.** Kiasi kitakachowekwa ni jumla ya shilingi **98,000/=. Lipa kuanzia Tarehe 01/07/2022.**

**NB: HAKIKISHA UNAWASILISHA RISITI YA MALIPO OFISI YA MHASIBU MARA UTAKAPORIPOTI SHULENI. RISITI IWE IMEANDIKWA JINA LA MWANAFUNZI NA MCHEPUO ANAOSOMA PAMOJA NA NAMBA YA SIMU YA MZAZI.**

**VIFAA VYA KUJA NAVYO SHULENI**

1) Ream 1 A4 – kwa ajili ya photocopy (e.g Nopa au Mondi)

   **NB:** Karatasi hizi kwa ajili ya mitihani ya wiki, mwezi na mwisho wa muhula kwa mwaka mzima na zitapokelewa katika ofisi ya Taaluma.

2) Vifaa vya usafi, wanafunzi wote wanatakiwa kuleta vifaa vya usafi kama ifuatavyo:-

   i) Soft broom, Hard Broom na Slasher vitakavyoletwa na HGK

   ii) Jembe lenye mpini na ndoo vitakavyoletwa na HGL

**SHERIA KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kutii sheria za shule, kuzingatia taratibu zote zilizowekwa pamoja na kufuata maelezo anayopewa na walimu wake.

**VAZI RASMI LA SHULE**

Kila mwanafunzi atalazimika kuvaa vazi la shule wakati wote anapokuwa katika eneo la shule na nje kwa shughuli za kishule. Kijana wa kiume anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote na kijana wa kike anatakiwa kuwa na nywele fupi au kusuka nywele kuanzia 5-7 wakati wote anapokuwa shuleni.

**4.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**4.1 Sare ya shule**

a. Sare ya shule
   2. Suruali (2) Dark Blue shati 2 nyeupe mikono mirefu na Tai Rangi ya suruali kwa wavulana
   3. Sketi (2) Dark Blue na blauzi mikono mirefu
   4. Nusu kanzu (shati) (2) kwa wasichana wa kiislamu (Sample ya kitambaa inapatikana shuleni).
b. Sare ya michezo kwa shule hii ni T- shirt Form Six (Maroon) kwa wavulana na wasichana, itakuwa inavaliwa siku ya Ijumaa tu na itapatikana shuleni.
c. Rangi ya Hijabu ni Nyeupe **ISIYO NA UREMBO**
d. Mkanda mweusi kwa wavulana.
e. Viatu vyeusi vya ngozi soli fupi, kwa wavulana vyenye kamba na wasichana muundo wa Juma na Roza, Soksi ndefu nyeupe kwa wasichana na soksi fupi nyeusi kwa wavulana, sweta rangi ya damu ya mzee (Maroon) yenye kola ya V (Vshape) kwa wote **(HARUHUSIWI KUVAA RANGI NYINGINE, AKIVAA ATANYANG'ANYWA NA HATARUDISHIWA)**

**NB**: **Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa vitu vifuatavyo akiwa katika sare ya shule kwa mfano bangili, pete, hereni, mkufu, "bronches" soksi, viatu tofauti na sare ya shule vitu hivi vikivaliwa, vikinyang'anywa havitarudishwa.**

**4.2. MAHITAJI MUHIMU**

**MENGINEYO YALETWE WAKATI WA USAJILI**

i. **Aje na Result Slip na Leaving Certificate bila kukosa original na nakala wakati wa usajili (MUHIMU SANA)**
ii. Picha nne(4) za rangi za passport size za mwanafunzi na moja ya mzazi au mlezi akiwa amevaa sare ya shule.
iii. Cheti cha kuzaliwa (Kivuli)
iv. Medical Examination Form imeambatishwa nyuma ya forms ambavyo itajazwa na mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
v. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai.
vi. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na kiapo kwa mzazi (imeambatishwa nyuma ya fomu) mahitaji muhimu mwanafunzi anatakiwa awe navyo
   a. Madaftari makubwa 9 (Counter 3 Quire)
   b. Madaftari madogo 9 (Msomi)
   c. Begi jeusi la kubebea vifaa vya shule
   d. Kalamu za kutosha za wino na penseli
   e. Rula ya cm 30 na kifutio
   f. Kamusi ya Kiswahili Sanifu – Oxford (**HGK**) na Dictionary ya Advance Learners kwa (**HGL**)
   g. Mathematical Set na **GRAPH PAD 2** kwa kila mwanafunzi.

**MUHIMU**

Ni lazima mwanafunzi afike shuleni siku iliyopangwa. Mimi pamoja na Jumuiya ya Aboud Jumbe Sekondari tunakupongeza sana kwa kuchaguliwa kujiunga na shule hii. Tunaamini utatoa ushiriano na mchango katika kuiendeleza Aboud Jumbe kielimu na kijamii kwa manufaa yako, shule na Taifa kwa ujumla.

**TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO / MAELEKEZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU**

**NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA**

……………………………………………………

**ROSE THOMAS MKONO**
**MKUU WA SHULE**

**MAWASILIANO**

**MKUU WA SHULE – 0784 344 495**

**MAKAMU – 0653 878 796 / 0716 014 044**

**MTAALUMA – 0719 139 913**

KIAMBATISHO A.

## FOMU YA KUKUBALIWA KUJIUNGA NA AHADI (1)

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI ABOUD JUMBE

S. L. P 10956

**DAR ES SALAAM**

**KWA MWANAFUNZI**

Mimi …………………………………………………………………………………………………… (Jina kamili)

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha ……… mwaka …… katika shule ya sekondari Aboud Jumbe.

**NINAAHIDI KWAMBA**

1. Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma
2. Nitaweka bidii katika masomo, kazi na shughuli zote kisheria.
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli zote, bila kuitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza mali za shule.
4. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya Shule ya Sekondari Aboud Jumbe.
5. Nitasoma kwa bidii zangu zote kuhakikisha ninafaulu na kupandisha ufaulu wa shule.

**MUNGU NISAIDIE**

**Saini ya Mwanafunzi ……………………………………………..TAREHE……………………**

**KIAMBATISHO B.**

**FOMU YA KUKUBALIWA KUJIUNGA NA AHADI (2)**

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI ABOUD JUMBE

S. L. P 10956

**DAR ES SALAAM**

**KWA MZAZI / MLEZI**

Mimi (Jina la mzazi / mlezi) …………………………………………………..

Mzazi / Mlezi wa …………………………………………………………………

**NINAAHIDI KWAMBA**

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yaliyotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule.
2. Nitalipa ada na michango ya shule kwa wakati pasipo kukwamisha shughuli za uendeshaji wa shule.
3. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajiwa(Maoni, adhabu, katika kumlea mwanangu kipindi chote awapo shuleni
4. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani(Home work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake kishule
5. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake
6. Nitahakikisha mwanangu hafiki na simu shuleni wakati wote.
7. Nitahakikisha anahudhuria shuleni siku zote za masomo panapotokea dharula nitatoa taarifa siku ya tukio.

**JINA** ……………………………………………….**SAHIHI** ………………**NAMBA YA SIMU** ……………………….

**KIAMBATISHO C**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

**SHULE YA SEKONDARI ABOUD JUMBE**

**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE**

**PICHA YA MWANAFUNZI**

**A. IJAZWE NA WANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi……………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………
3. Taifa………………………………………………………………………………
4. Uraia………………………………………………………………………………
5. Dini…………………………………………………………………………………
6. Shule za sekondari alizosoma kabla ya kuja shule ya Sekondari Aboud Jumbe

| SHULE YA SEKONDARI | TAREHE NA MWAKA ULIOAANZA | TAREHE NA MWAKA ULIOMALIZA |
|---|---|---|
| i. ……………………………………… | ……………………………………………….. | ……………………………………………… |
| ii.…………………………………… | ……………………………………………… | ……………………………………………… |
| iii. ………………………………… | ……………………………………………… | ……………………………………………… |
| iv. ………………………………… | ……………………………………………….. | ……………………………………………... |

Saini ya mwanafunzi ………………………………………………………… Tarehe ………………………..

**B. Maelezo ya binafsi ya mzazi / mlezi**

**PICHA YA MZAZI / MLEZI**

1. Jina kamili la mzazi / mlezi …………………………………………………………………...
2. Utaifa ………………………………………………………………………………….........
3. Uraia ……………………………………………………………………………………......
4. Sehemu anayoishi …………………………………………………………………….........
5. Mtaa ……………………………………………….… Kata ……………………………......
6. Namba ya nyumba …………………………………………………………………….……
7. Simu: Nyumba …………………………………………………………………………………
   Ofisi …………………………………………………………………………………
   Barua pepe ……………………………………………………………………………..
8. Mtendaji / Mwenyekiti wa mtaa . Jina …………………………… Sahihi ……………Mhuri……………..
   Simu ……………………………..
9. Mjumbe. Jina …………………………… Sahihi …………… Mhuri …………….
   Simu ……………………………..

Elezea kama mtoto ana matatizo yoyote ya kiafya…………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………...

**C. MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI / MLEZI**

Kazi ya mzazi / mlezi ……………………………………………………………………………………….

**KIAMBATISHO D.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**KIGAMBONI MUNICIPAL COUNCIL**
**ABOUD JUMBE SECONDARY SCHOOL**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**DATE: ……………………………**

**PART A:**
To:
Medical Officer
…………………………………………………………………………………………………………………..…
……………………………………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………………………..…
……………………………………………………………………………………………………………………..
Miss / Mr ……………………………………………………………………………………………………….…

Please examine the above named student fitness for admission:-

Put(V) for positive and a cross (x) for a negative against in a box provided

| | |
|---|---|
| Pregnancy | (   ) |
| Asthma | (   ) |
| Sight | (   ) |
| Diabetes | (   ) |
| Worm (Stool) | (   ) |
| Epilepsy | (   ) |
| TB (Tuberculosis) | (   ) |
| Sickle cell | (   ) |
| Heart disease | (   ) |
| Yellow fever | (   ) |
| U.T.I | (   ) |
| Malaria | (   ) |

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named student and consider that he / she is physically **FIT/ UNFIT** for admission as above.

**Name: …………………………………………… Signature ……………………… Date …………………….**

**Station ………………………………………….. Destination ……………………………….....**

**Officia stamp ……………………………………………….…………….**

**KIAMBATISHO E.**

**SHULE YA SEKONDARI ABOUD JUMBE**

**MSHONO WA SKETI NA SURUALI YA MWANAFUNZI**

**MBELE**




**NYUMA**




**NB:** Mshono wa sketi ni **''A'' Shape** na siyo **''Solo'' au ''Tight'' iwe ndefu isiyobana inayovuka magoti.**

**MBELE**



**NYUMA**



**NB:** Mshono wa suruali usiwe ''**MODO'' Upana wa suruali chini uwe kati ya cm 17**

## SHULE YA SEKONDARI ABOUD JUMBE

### ORODHA YA VITABU- KIDATO CHA TANO NA SITA

**1. KISWAHILI**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Nadharia ya Lugha | Masebo, J. |
| ii. | Kiswahili Kidato cha 5 &6 | Oxford University Press |
| iii. | Nadharia ya Fasihi | Masebo, J. |
| iv. | Tahakiki | Masebo, J. |
| v. | Nadharia ya Lugha Kidato cha tano | Christopher Masuko, |
| vi. | Tahakiki Kidato cha Tano na Sita | Masebo, J. |
| vii. | Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita Kiswahili II 4. TIE | |
| viii. | SARUFI MAUMBO YA KISWAHILI | SAMIKISA |

**Vitabu fasihi Riwaya :**

i. Vuta ni Kuvute,

ii. Mfadhili,

iii. Usiku utakapokwisha na kufikirika.

**Tamthiliya:**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Ukingo wa Thimu, | |
| ii. | Kufikilika | Shaban Robert |
| iii. | Nguzo Mama, | |
| iv. | Kivuli kinaishi na MORANI | |

**Ushairi :**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Kimbunga, | |
| ii. | Fungate ya uhuru, | |
| iii. | Chungu Tamu na Mapenzi 5. | |
| iv. | Miundo ya Kiswahili sanifu | SAMIKISA |
| v. | Nadharia ya Lugha ya Kiswahili kilichoandikwa | P. Saluhaya |

**2. ENGLISH LANGUAGE**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Advanced English Language | Oxford |
| ii. | English Language | Nicholaus Ashel |
| iii. | Literature in English | |
| iv. | Advanced Level Literature | Nyambari Nyangwine 2010 |
| v. | Advanced Level English | Francis Mnyari (2014) |
| vi. | Intoduction to Language and other books for A level | Michael Kadeghe. |

**Poems TIE.**

i. Selected Poems
ii. Wonderful Surgeion — Charles Mloka
iii. Summorns

**Plays:**

i. I will mary when i want, — Lwanda Magere,
ii. Betrayal in the city
iii. An enemy of the people

**Novel:**

i. A man of the people,
ii. A beatifuly one are not yet born
iii. His excelency the head of the state

**NB: And Other A- LEVEL books .**

**3. GEOGRAPHY**

i. Physical Geography(01) — D T Msabila
ii. Human Economic Geography (02) — D.T Msabila
iii. Prichard J.M. (1990) Practical Geography for Africa Longman.
iv. Kamili, 2, Physical Geography for Africa Dar es salaam Afroplus Industries.
v. Map Reading, Photography Enterpretation and Elementary Suveying — D.M .Master.
vi. Research Methodology, Methods and Technique — C . R Kothari
vii. Afica in Focus Physical Human and Economic Geography Revised EDITION — Richard White.

**4. HISTORY**

i. Mastering Advance Level History Book One & Two By Mwl. Kato A. Kassim
ii. Contemporary Historical Events by Comrade C. K Shibiliti
iii. Basic themes in Advanced level History paper One by Flore M. Mavunde
iv. Lesson Notes for Advanced Certificate of Secondary Education by Mwl. Bakari Madaya (2018)
v. Essentials in Advanced Level History Paper 1 & 2 — Saleh Yassin

**5. GENERAL STUDIES**

i. Nyambari Nyangwine, G. Bukagile and S.O. Maluka.(2010) Contemporary Approach for Advanced Level-General Studies notes form Five and Six
ii. Bigirwamungu J. and Deogratius S. M (2012) Understanding General Studies For Advanced Level Certificate
iii. Richard R.F Mbalase (2012) General Studies for Advanced Level Cetificate Afroplus Industries (T) Ltd

**<u>NB: *Ni muhimu kila mwanafunzi kuja na vitabu vya TAHASUSI anayosoma*</u>**